

MWONGOZO WA KUSAHIIHISHA 102/1 – INSHA **KIDATO CHA NNE MUHULA 2 2024**

1. Hii ni insha ya ripoti maalum
Vipengele vifuatavyo vijitokeze

a) Muundo

- i. Kichwa
Kichwa kitaje kuwa ni ripoti ya jopo au kamati
Kichwa kionyeshe suala linaloshughulikiwa
Kitaje mahali pa uchunguzi
Mwaka wa kuandikiwa ripoti hutajwa
- ii. Utangulizi
Utangulizi utaje:
Usuli wa jambo
Wadhamini
Malengo na majukumu ya wanajopo
Muda ambao ripoti itachukua
Majina ya wanajopo
- iii. Mbinu za ukusanyaji wa data
- iv. Mwili wa ripoti-matokeo ya uchunguzi
- v. Hitimisho
- vi. Mapendekezo
- vii. Sahihi
- viii. Jina
- ix. Cheo/wadhifa



b. Maudhui

Hoja zifuatazo ziweze kujitokeza (matokeo)

- i) Shinikizo kutoka kwa wazazi ambao wanataka watoto wao kuupasi mtihani
- ii) Nafasi chache katika vyuo vikuu husababisha ushindani mkubwa
- iii) Utovu wa maadili mionganoni mwa wanafunzi
- iv) Ukosefu wa sera madhubuti kuhusu mitihani
- v) Walimu kujihusisha na undanganyifu
- vi) Wasimamizi wa mitihani kuzembea
- vii) Wasimamizi kupokea mlungula na kuruhusu undanganyifu
- viii) Ushindani baina ya shule mabalimbali
- ix) Jamii kuona kuwa kufeli mtihani kama mwisho wa maisha
- x) Mfumo wa elimu kuweko msisitizo mkubwa katika kuupasi mtihani.
- xi) Maendeleo ya kitechnolojia

Mapendekezo

- i. Wazazi kutoshinikiza watoto wao
- ii. Nafasi katika vyuo vikuu zipanuliwe
- iii. Wanafunzi wafunzwe maadili
- iv. Sera madhubuti ziwekwe
- v. Onyo kali kwa walimu wanaojihusisha na udanganyifu
- vi. Hatua kali zichukuliwe kwa wale wanaopokea hongo
- vii. Mfumo wa elimu kubadilishwa

Tanbihi

- i. Mtahiniwa awe na hoja nane na zaidi ili kujitosheleza kimaudhui
- ii. Mtahiniwa akikosa sura ya ripoti aadhibiwe kwa kutolewa alama nne za sura **4S**

2. Hii ni insha ya maelezo

Baadhi ya hoja ni:

- i. Serikali kutangaza baa la njaa kama kama janga la kitaifa
- ii. Kutoa misaaada kwa wahasiriwa wa njaa
- iii. Wakulima kuhimizwa kupanda vyakula vinavyostahimili kiangazi
- iv. Serikali kutenga pesa ili kuwezesha shirika la nafaka nchini kununua na kuhifadhi mazao.
- v. Kutoa njia bora za ukulima kwa wakulima
- vi. Kupunguza bei ya pembejeo
- vii. Wakulima kupewa ruzuku ya kifedha ili kuendeleza kilimo
- viii. Kununua mazao kutoka kwa wakulima kwa bei nzuri ili kuwapa motisha wakulima.
- ix. Kuwaajiri maafisa wa kilimo nyanjani ili kuwafikia wakulima
- x. Kuhamasisha vijana kushiriki kilimo badala ya kuhamia mjini kutafuta kazi
- xi. Wananchi kuhimizwa kuhifadhi mazingira

Tanhibi

Mtahiniwa awe na hoja nane na zaidi ili kujitosheleza kimaudhui

3. Hii ni insha ya methali. Mtahiniwa atunge kisa kinachobainisha maana ya methali. Maana ya methali ni kuwa mzazi asiporekebisha uovu wa mwana akiwa mdogo itakuwa vigumu kumrekebisha akiwa mkubwa.

Itakuwa kazi ngumu sana kumrekebisha akiwa mkubwa. Pia jambo lolote lile lafaa kurekebishwa katika hatua za mwanzo. Itakuwa vigumu kulirekebisha likiwa limezidi

Ruwaza zifuatazo zinaweza kujitokeza

- i) Mzazi akose kumrekebisha mtoto akiwa mdogo na imgharimu sana kujaribu kumrekebisha akiwa mkubwa
- ii) Jambo fulani lipuuziliwe kurekebishwa mapema halafu ligharimu sana kulirekebisha baadaye

Tanbihi

- i. Mtahiniwa aonyeshe pande zote mbili za methali
 - ii. Mtahiniwa akitunga kisa kisichoana na methali atakuwa amepotoka kiandhui. Apate D 03
4. Hii ni insha ya mdokezo wa kumalizia. Mtahiniwa atunge kisa ambacho kitooana na mdokezo aliopewa. Kisa kionyeshe masimulizi ambayo yatadhihirisha kitendo ambacho mhusika alifanyiwa cha kuaibishwa. Kwa vyovyyote vile kisa kiwe ni aibu ambacho kinamuaibisha mhusika. Kisa kinawenza kuhusu labda maovu ambayo mhusika alikuwa akifanya halafu yakaanikwa mbele ya hadhara

Tanbihi

- i. Mtahiniwa akitunga kisa ambacho haioani na mdokezo atakuwa amepotoka kimaudhui
- ii. Mtahiniwa akikosa kuandika mdokezo atakuwa amepungukiwa tu kimitindo